**KARIBU: Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia uwekezaji, Angella Kairuki, akizungumza na wafanyakazi wa kampuni ya kuzalisha nguzo za umeme ya Qwihaya General Enterprises mkoani Iringa juzi.**

MTANZANIA UK 2.

# Kairuki avutiwa uwekezaji kiwanda cha kuku, kilimo

**Na MWANDISHI WETU**
-IRINGA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki amevutiwa na uzalishaji wa chakula cha kuku, ufugaji wa kuku pamoja na mbogamboga katika Kongani ya Ihemi kwenye ushoroba wa Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) na kusema kuwa uwekezaji huo unakwenda sambamba na azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2015.

Hayo aliyasema jana mjini hapa baada ya kutembelea kwa nyakati tofauti viwanda vya Silverlands, Masifio Estates, Pyrethrum Tanzania (PCT), Qwihaya General Entreprises na Sao Hill.

Kairuki alisema kuwa uwekezaji wa kuku na kilimo cha mbogamboga katika eneo hilo una mchango mkubwa katika kuongeza kipato kwa wakazi wa Iringa.

"Nimevutiwa sana na uwekezaji huu wa kiwanda cha kutengeza chakula cha kuku, ufugaji wa kuku na kilimo cha mbogamboga. Kama Serikali tutaendelea kuboresha na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji hapa nchini.

"Hii siyo hadithi, nimejionea mwenyewe namna uzalishaji mkubwa wa kuku na mbogamboga unavyofanyika, na sisi kama Serikali tutahakikisha tunawaunga mkono ili kujenga na kuimarisha sekta husika pamoja kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi hapa nchini," alisema Kairuki.

Alisema kiwanda cha Silverlands kimekuwa chachu ya maendeleo kwa upande wa kuku, lakini pia wamekuwa wanunuzi wakubwa wa zao la mahindi kutoka kwa wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na hivyo kuliongezea thamani zao hilo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela alisema kuwa kiwanda cha Silverlands kimekuwa na mchango mkubwa na kuhakikisha maendeleo ya mkoa huo kwa kuwahakikishia wakulima soko la uhakika la mazao ya mahindi na soya.

---

**watakaowasili nchini wakati huu wa janga la corona.**

**Dk. Kigwangalla alisema kuwa Tanzania imezindua mwongozo wa taifa wa uendeshaji wa shughuli za utalii unaosimamia usalama na afya za wadau wote wanaojihusisha na sekta ya utalii wakati huu wa janga la corona.**

**Aliwahakikishia mabalozi hao kuwa watalii wote wanaowasili Tanzania katika kipindi hiki cha janga la corona wako salama kutokana na uwepo wa mwongozo huo unaolinda afya za wasafiri kuanzia kuwasili na kuondoka kwao.**

**"Mwongozo huu unatoa usimamizi kwenye viwanja vya ndege, hoteli za kitalii, watoa huduma za utalii, upimaji wa afya za wahudumu na wageni wote wanaoingia nchini pamoja na ukusanyaji wa taarifa za wasafiri wote wanaoingia nchini Tanzania," alisema Dk Kigwangalla.**

Scanned with CamScanner

## wajane

mefanikisha wajane kuwa kitu kimoja na hasa kushauriana mambo mbalimbali ya maendeleo.

Alisema pia umewasaidia utambulika serikalini na kupata misaada na mikopo ya fedha kuendesha maisha yao.

Mwanasheria kutoka Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) - Tanzania, Zakia Msangi alisema sheria ya mirathi ya kimila inahitaji kufanyiwa marekebisho kwa sababu ina upungufu mwingi.

Moja ya upungufu huo, alisema ni kutokuweka muda maalumu wa usikilizaji wa mashauri ya mirathi.

"Sheria inaweka hitaji la lazima la kuwepo kwa muhtasari wa kikao cha ndugu, ni tatizo kwa kuwa mara nyingi kunakuwa na ugomvi baina ya ndugu wa marehemu na mke wa marehemu, hivyo kusababisha kushindwa kufikia mwafaka, mjane kutengwa na hata kufukuzwa katika vikao," alisema Zakia.

# Mtuhumiwa sugu wa mauaji mbaroni

**Na ALLAN VICENT**
-TABORA

MTUHUMIWA sugu wa mauaji na uvunjaji nyumba aliyekuwa akisakwa kwa muda mrefu na Jeshi la Polisi mkoani Tabora, amekamatwa kutokana na msako mkali uliofanywa maeneo mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Barnabas Mwakalukwa alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa kutokana na ushirikiano mzuri wa wananchi kwa jeshi hilo.

Alimtaja mtuhumiwa kuwa ni Juma Nassibu, maarufu 'Juma Macho' na kwamba anaendelea kuhojiwa.

Kamanda Mwakalukwa alisema msako unaendelea kwa weledi mkubwa maeneo yote ya mkoa hadi hapo wenzake watakapokamatwa au kujisalimisha wenyewe.

Alisema katika msako huo, pia walifanikiwa kumkamata kinara wa wizi wa pikipiki mwenye mtandao mpana mikoa ya Tabora, Mwanza, Shinyanga na Mara.

Kamanda Mwakalukwa alisema baada ya mahojiano na polisi, mtuhumiwa alikiri kuhusika na mtandao huo wa wizi wa bodaboda na kubainisha tayari ameiba zaidi ya nane katika mikoa hiyo.

Baada ya kukamatwa, alikutwa na vitu mbalimbali ikiwemo pikipiki tatu zenye namba za usajili T 615 AVE aina ya SanLG, MC 977 AAB na T 791 ATN, huku pikipiki yenye nambari MC 274 ikiwa inabadilishwa injini yake.

Alitaja vitu vingine ni radio sabwoofer moja, TV tatu flat screen, deki moja, baiskeli mbili na magodoro mawili.

**ONYO**



# Watumia vyandarua kuvulia samaki

**Na GURIAN ADOLF**
-KALAMBO

**BAADHI ya wakazi waliopo vijiji vya mwambao wa Ziwa Tanganyika mkoani Rukwa, wamekuwa wakitumia vyandarua vinavyotolewa bure na Serikali kwa wajawazito na watoto kujikinga na malaria kuvulia samaki.**

**Wakizungumza na gazeti hili jana, baadhi ya wakazi hao walidai wamekuwa wakitumia vyandarua katika shughuli za uvuvi, kilimo na ufugaji kwa kuwa nyavu maalumu za shughuli hizo hazipatikani wilayani humo.**

**Mmoja wa wakazi hao, Rosemary Mtepa alisema baadhi wamekuwa wakitumia vyandarua kutega samaki Ziwa Tanganyika, wengine wakivitumia kuzungushia bustani ili kuzuia kuku kuingia na kuharibu mazao yao.**

**Alisema pamoja na kutambua nia ya Serikali kuwapa wajawazito vyandarua hivyo, wamekuwa wakipuuza matumizi hayo na badala yake kutumia katika matumizi wanayoyojua wenyewe.**

**Diwani wa Kata ya Kasanga, Jacob Chisenga alikiri kuwapo matumizi mabaya ya vyandarua.**

**Alisema limekuwa tatizo kubwa ambalo linawasumbua wakazi wa eneo hilo la mwambao mwa ziwa.**

**Chisenga alisema elimu ya matumizi ya vyandarua bado inahitajika eneo hilo kama njia ya kuwasaidia wananchi kukabiliana na malaria.**

**Ofisa Afya Wilaya ya Kalambo, Richard Manuma alisema kipindi hiki ambacho wameanza kuandikisha majina kwenye kaya, kila moja itapewa vyandarua viwili.**

Scanned with CamScanner

NIPASHE · UK 5.

# Kairuki avutiwa uwekezaji kiwanda cha kuku, mboga

**Na Mwandishi Wetu, IRINGA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, amevutiwa na uzalishaji wa chakula cha kuku, ufugaji wa kuku pamoja na mboga katika Kongani ya Ihemi kwenye ushoroba wa Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT).

Amesema uwekezaji huo unakwenda sambamba na azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Nimevutiwa sana na uwekezaji huu wa kiwanda cha kutengeneza chakula cha kuku, ufugaji wa kuku na kilimo cha mboga. Serikali tutaendelea kuboresha na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji nchini," alisema Waziri Kairuki.

Akizungumza kwa nyakati tofauti jana alipotembelea kiwanda cha ufugaji na uzalishaji wa chakula cha kuku cha Silverlands, Masifio Sstates, Pyrethrum Tanzania (PCT), Qwihaya General Entreprises na Sao Hill, Waziri Kairuki alisema uwekezaji wa kuku na kilimo cha mboga katika eneo hilo una mchango mkubwa katika kuongeza kipato kwa wakazi wa Iringa.

" Hii siyo hadithi, nimejionea mwenyewe namna uzalishaji mkubwa wa kuku na mboga unavyofanyika, na sisi kama serikali tutahakikisha tunawaunga mkono ili kujenga na kuimarisha sekta husika pamoja kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi nchini," alisema.

Alisema kiwanda cha Silverlands kimekuwa chachu ya maendeleo kwa upande wa kuku, lakini pia wamekuwa wanunuzi wakubwa wa zao la mahindi kutoka kwa wakulima wa mikoa ya nyanda za juu kusini na hivyo kuliongezea thamani zao hilo.

Waziri Kairuki alionyesha pia kufurahishwa na kilimo cha mboga katika shamba la Sasifio, akisema kimetoa mchango mkubwa wa kukidhi mahitaji ya mahoteli pamoja na sekta ya utalii kwa kuzalisha aina 14 za mboga ambazo nyingi awali zilikuwa zikiagizwa kutoka nje ya nchi.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, alikipongeza kiwanda cha Silver Lands kwa mchango wake katika maendeleo ya mkoa kwa kuwahakikishia wakulima soko la uhakika la mazao ya mahindi na soya.

Naye mwekezaji katika shamba la Masifio, Quitin Robb alikipongeza Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuhakikisha mazingira ya uwekezaji yanakuwa rafiki.

HABARI LEO UK 4.



ari ya Dar es
ake ni Naibu
wa bandari hiyo

# gozo
# Dar

gumzia hilo kisha
ayo itatoa waraka huo
ambao kila gari kutoka
rani itapaswa kutozwa
a Marekani 500 isi-
va tu kwa magari ya
da yale yanayoingia
Bandari ya Dar es
n.
ati namba moja na
ambazo zamani
gwa kwa msaada wa
li ya Ubelgiji, hivi sasa
aba huo unaisha kwa
u badnari hiyo kwa
a iko kwenye mabore-
alifafanua.
vi karibuni Chama cha
iliki wa Malori (TATO)
lamikia tozo hiyo ya
i kwa kusema Rwanda
ewa upendeleo na
lipa dola 152 wakati
yingine zinalipa Dola
a kutaka kuwepo na
a.

## a bidhaa

buzi.
moja na kuidhinisha
gozo huo, baraza hilo
metambua kazi kubwa
fanywa na made-
a utingo wa malori
a kusafirsha bidhaa
duma muhimu katika
di chenye changamoto
vid-19.
lisema kama madereva
ingo wasingesafirisha
a na huduma muhimu,
i ambalo lingeathirika
kiasi kikubwa ni wanan-
Alisema pamoja na uja-
uo wa madereva, SADC
azingatia tahadhari
opaswa kuchukuliwa ili
anusuru na maambukizi
rusi vya corona.

# Waziri avutiwa ufugaji wa kuku

**Na Mwandishi Wetu, Iringa**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki amevutiwa na uzalishaji wa chakula cha kuku, ufugaji wa kuku pamoja na mbogamboga katika Kongani ya Ihemi kwenye ushoroba wa Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) kwani amesema uwekezaji huo unakwenda sambamba na azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Nimevutiwa sana na uwekezaji huu wa kiwanda cha kutengeza chakula cha kuku, ufugaji wa kuku na kilimo cha mbogamboga. Kama serikali tutaendelea kuboresha na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji hapa nchini," alisema Kairuki.

Akizungumza kwa nyakati tofauti jana alipotembelea Kiwanda cha ufugaji na uzalishaji wa chakula cha kuku cha Silversands, Masifio Estates, Pyrethrum Tanzania (PCT), Qwihaya General Enterprises na Sao Hill, alisema uwekezaji wa kuku na kilimo cha mbogamboga katika eneo hilo una mchango mkubwa katika kuongeza kipato kwa wakazi wa Iringa.

"Hii siyo hadithi nimejionea mwenyewe namna uzalishaji mkubwa wa kuku na mbogamboga unavyofanyika, na sisi kama serikali tutahakikisha tunawaunga mkono ili kujenga na kuimarisha sekta husika pamoja kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi hapa nchini," alisema.

Alisema kiwanda cha Silverlands kimekuwa chachu ya maendeleo ya kuku lakini pia kimekuwa mnunuzi mkubwa wa mahindi kutoka kwa wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na hivyo kuliongezea thamani zao hilo.

"Napongeza uongozi wa kiwanda cha Silverlands kwa kazi nzuri wanayofanya kuhakikisha wanawainua wakulima na wakazi wanaozunguka eneo la mradi pamoja na kutoa ajira kwa kwa vijana," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela amekipongeza kiwanda cha Silversands kwa mchango wake katika maendeleo ya mkoa kwa kuwahakikishia wakulima soko la uhakika la mazao ya mahindi na soya.

Scanned with CamScanner

Jiji la Arusha pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqqaro.

hilo, Homera alisema miili ya watoto wawili waliozaliwa wafu na kuhifadhiwa chumba

mwaka saa 11 ambako muuguzi msaidizi alimtaarifu kuwa miili ya watoto wawili walio-

na uchungu wa uzazi uliodumu hadi saa 11 jioni ambako alikimbizwa hospitalini hapo

mkoa imsaidie aupate mwili wa marehemu mwanawe ili wakausitiri.

HABARI LEO

# Bwawa la Julius Nyerere kuongeza ulaji samaki

**Na John Nditi, Morogoro**

ULAJI samaki kwa Watanzania utaongezeka kutoka wastani wa kilo 8.2 kwa mtu mmoja kwa mwaka hadi kufikia kilo 20 baada ya kukamilika ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere wilayani Rufiji, Pwani.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Rashid Tamatamah (Uvuvi) alisema hayo hivi karibuni wakati wa ziara ya makatibu wakuu na naibu makatibu walipotembelea ujenzi wa mradi huo wilayani Rufiji, unaosimamiwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO). Utazalisha megawati 2,115 za umeme.

Dk Tamatamah alisema sekta ya uvuvi itafaidika na kujengwa kwa bwawa hilo kwani licha ya kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme nchini, litatoa fursa kubwa kwa walaji wa samaki kutokana na kuongezeka kwa samaki.

"Ulaji wa samaki kwa sasa ni kilo 8.2 kwa mtu mmoja kwa mwaka na hilo lipo chini sana kulingana na takwa lililowekwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), kuwa ulaji wa samaki ni kilo 20 kwa kila mtu mmoja kwa mwaka," alisema Dk Tamatamah.

"Ukichukulia wastani kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ni kama kilo kumi za samaki kwa kila mtu mmoja kwa mwaka kiwango ambacho ni cha chini sana," alisisitiza Dk Tamatamah.

Katibu Mkuu alisema mkakati wa uliowekwa na wizara katika miaka minne hadi mitano ijayo ni kuhakikisha ulaji wa samaki unaongezeka hadi kufikia kilo 10 kwa mtu mmoja kwa mwaka.



Pamoja na hayo, alisema kwa sasa uzalishaji wa samaki nchini umefikia tani 448,000, na endapo utaongezeka kufikia tani 700,000, kuna uwezekano mkubwa ulaji wa samaki kufikia lengo lililowekwa na FAO. Alitaja mkakati mwingine uliochukuliwa kwenye Ziwa Victoria ni wa kusimamia na kukomesha uvuvi haramu na hatua hiyo imewezesha samaki kuanza kuongezeka pamoja na watu wengi wameingia kwenye ufugaji samaki.

Alisema licha ya kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki katika ziwa hilo, zilijitokeza changamoto nyingine zikiwemo za miundombinu na bei ya samaki kushuka na wavuvi kutopata thamani ya jasho lao.

"Tulichokifanya mwaka jana (2019) baada ya ongezeko la uzalishaji wa samaki kwenye ziwa hilo ni kuhamasisha watu na sekta binafsi kujenga maghala na kuhifadhi na kugadisha samaki. Mwaka 2017 yalikuwepo maghala nane pekee na kwa sasa 2020 kuna maghala 90 yenye uwezo wa kila moja kuhifadhi kwa siku kilo 350," alisema.

Hivyo alisema umeme utakaozalishwa kutoka kwenye Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere utasaidia kuanzisha maghala mengine sehemu mbali mbali hadi vijijini na samaki watafikishwa maeneo hayo kitendo kitakachochangia kuongeza kiwango cha ulaji wa samaki.

HABARI LEO UK 20.

# Waziri Mifugo ateua Wajumbe Bodi ya LITA

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina amemteua Profesa Malongo Mlozi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala ya Vyuo vya Mifugo Tanzania (LITA).

Kwa mujibu wa taarifa ya Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano serikalini wa wizara hiyo, Rehema Mbulalina, pia Mpina amewateua wajumbe wa Bodi ya LITA ambao ni Profesa Zacharia Masanyiwa, Mark Tsoxo, Josephine Matiro na Faraja Makafu.

Taarifa hiyo ya Mbulalina ilieleza kuwa uteuzi huu umeanza Juni 20, mwaka huu na bodi itazinduliwa Julai 6, mwaka huu katika Ofisi za Serikali Mtumba jijini Dodoma.

Aidha, taarifa hiyo iliwataja wajumbe wanaoingia katika bodi kwa nafasi zao ni Dk Angello Mwilawa ambaye ni Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani na Dk Pius Mwambene ambaye ni Mtendaji Mkuu – LITA.

Po
m

Na Jose

K
wazazi
kuwa m
desturi
ngoma
na mitar
zinachoo
sia ukiw
wanawa
Kamar
Kamishn
alisema h
wa warsh
sa wa pol
Kipolisi
fisa wa u
mahakim
huduma

Kar

shwa katika mradi huo na katika kipindi chote cha uongozi wake

anasema hakuna kinachoendelea na kwamba wananchi wake wali-

"Tathimini iliyofanyika jamani ni ya ajabu, watu hatujashirikishwa tangu mwanzo, waliwadanganya wanan-

mwaka 2010 uliokuwa umelenga kuwapatia ajira lukuki vijana.

mradi wanaodaiwa kufeli.

UFUGAJI

# VTLA waja na njia kuongeza idadi ya mifugo

Aurea Simtowe, Mwananchi
asimtowe@mwananchi.co.tz

Wafugaji sasa huenda wakapata ahueni na kuongeza idadi ya mifugo yao baada ya Wakala wa Vetinari (VTLA) kupata namna wanayoweza kudhibiti kuharibika kwa mimba za mifugo hasa ng'ombe.

Hatua hiyo imekuja baada ya kusaini mkataba wa makubaliano na Kampuni ya Uhimilishaji Afrika Mashariki (ABEA) utakaowezesha upimaji wa sampuli za wanyama kwa haraka ili kubaini ugonjwa huo ambao kitaalamu huitwa brucellosis kwa kutumia kifaa kiitwacho Fluorescent Polirization Assay (FPA).

Mtendaji mkuu wa TVLA, Dk Furaha Mramba anasema kabla ya mkataba huo walikuwa wakitumia hadi siku tatu kusubiri majibu ya sampuli walizopima tofauti na sasa wanatumia dakika tano.

"Licha ya kusubiri siku hizo lakini pia tulikuwa hatuna uhakika na majibu yanayotolewa, sasa wafugaji wakae mkao wa kula kwa sababu tutadhibiti kwa kiasi kikubwa malalamiko ya mimba ya ng'ombe kuharibika na wao kujisikia vibaya," anasema Dk Mramba.

Pia, anasema ili kufanikisha suala hilo vipimo hivyo vitapelekewa katika maeneo yaliyo na ng'ombe wengi ikiwamo Mwanza, Arusha na Iringa kwa sababu ni mikoa inayozalisha maziwa mengi na maabara ya rufaa Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na VTLA, mwaka jana pekee asilimia 10 ya sampuli za ng'ombe 11,549 zilibainika kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo.

**Sh20,000**

**Bei ya kipimo cha sampuli kama ng'ombe mgonjwa**

Mkurugenzi wa uchunguzi wa magonjwa ya wanyama VTLA, Dk Henry Magwisha anasema mbali na ugonjwa huo kuathiri mifugo, pia huweza kuambukiza hadi binadamu. "Binadamu akiathiriwa na ugonjwa huu hupata homa za vipindi zilizo na dalili kama malaria na maabara chache ndiyo zinazoweza kugundua ugonjwa huo," anasema Dk Magwisha.

"Pia, matibabu yake ni ghali na asipoyapata kwa wakati huweza kupoteza maisha na kama ni mjamzito, mimba yake huweza kuharibika kutokana na homa kali za mara kwa mara. Hakuna dawa maalumu bali antibiotiki ndiyo hutumika kumtibu mtu."



Akizungumzia kifaa cha FPA anasema kinatumia sampuli aina mbili yaani maziwa na damu tofauti na kifaa cha awali kilichokuwa kinatumia damu pekee.

Mkurugenzi Mkuu wa ABEA, Masele Masunga anasema wafugaji sasa wanatakiwa kuachana na imani za kishirikina za kudhani ng'ombe wao wamerogwa kila mimba inapoharibika.

"Sisi huwa tunafanya uhimilishaji wa mifugo hasa ng'ombe na huwa tunakutana na changamoto hii sana, unahimilisha ng'ombe lakini baada ya muda mimba inatoka na mfugaji anakuwa haelewi ni kitu gani na kuhisi labda wanachezewa," anasema Masunga.

"Pia, kipimo hiki ni Sh2,000 kwa sampuli na mfugaji atajua kama ng'ombe wake ni salama na kama ana maambukizi basi ampatie chanjo."


Scanned with CamScanner

MWANANCHI UK 16.

Pngowi2002@yahoo.com.
0 754 653 740

a

# bajeti



dombinu laini.
ivyo, haina maana kuwa bajeti e katika miundombinu migumu.
ombinu laini wakati wa corona
una wakati ambao matumizi na ı wa miundombinu laini vime-ubwa zaidi ni wakati wa janga ı. Duniani kote shughuli nyingi o za kiuchumi zimehamia katika gu wa kidijitali. Hii ni kutokana ı zinazotumika kupambana na a kwa corona zikiwamo kufun-i mbalimbali na kufanyia kazi ni.
izi ya miundombinu laini e mitandao kuwezesha miku-somo, miamala mbalimbali ya na kadhalika yameongezeka ka kipindi cha corona.
uwa njia ya kudumu ya kufanya mbalimbali kwa sasa na muda ekeza katika wingi na ubora wa binu laini hakuepukiki.

**ombinu migumu**

usisha vitu kama barabara na yake, reli, viwanja vya ndege, mabwawa kwa matumizi li na kadhalika.
miundombinu muhimu sana umi wa nchi yoyote ile. Pamoja o mengine hufungua fursa za katika nchi husika.
nbinu hii ni muhimu sana kati-ı na kubakiza wawekezaji na ashara ndani ya nchi.
umbao uchumi umeingia zaidi nwengu wa kidijitali, miun-laini inazidi kuwa muhimu pengine kupita miundombinu



Aurea Simtowe

**KONA YA MMACHINGA**

# Muuza maziwa na ndoto ya kumiliki ng'ombe

Wakati mwingine unaweza kuendesha maisha yako kwa kufanya biashara ndogondogo nyingi na kukupa faida nzuri.

Hilo imeonekana kwa Yanga Omary (32) ambaye ameamua kuendesha maisha yake kwa kufanya biashara ya uuzaji sambusa, maziwa na mayai ya kienyeji.

Anasema alianza na biashara ya kuuza sambusa mwaka 2017 ambayo ndiyo iliweza 'kuzaa' biashara nyingine ndani ya muda mfupi.

"Niliuza sambusa kwa ajili ya mahitaji yangu madogo ya kujipatia kipato cha kula, sio kwa malengo lakini mwaka 2018 nilianza kufanya kazi hii kwa malengo ili izalishe biashara nyingine wakati huo nikiwa na mtaji wa Sh40,000," anasema Omary.

"Nilifanya hivyo na baada ya miezi saba nilitoa kiasi kidogo cha faida na kuanza kuuza maziwa ya fresh; miezi mitano baadaye nilitoa tena faida kidogo na kuanza kuuza maziwa mtindi.

**Lita 80**

Kiwango cha maziwa anayouza Omary kila siku

"Nikiwa na mtaji wa Sh15,000 nilianza kuuza maziwa fresh na baadaye kwa mtaji huo nilianza kuuza maziwa mtindi huku nikinunua lita 10 pekee. "Lakini mpaka sasa biashara yangu imekuwa na nina uwezo wa kununua lita 80 za maziwa kila siku; lita 40 nagandisha na mengine nauza huku nikiuza sambusa zaidi ya 100 kwa siku, jumla na rejareja," anasema Omary.

Pia, anasema baada ya kununua maziwa hayo huyaweka katika madumu ya lita tano na kuyauza kwa Sh13,500.

Omary anasema kupitia biashara hiyo amekuwa na uhakika wa kujipatia mahitaji yake ya kila siku na kuendeleza maisha yake licha ya kukutana na changamoto mbalimbali.

"Kuna wateja huwa sio waaminifu, anaweza kukuambia niletee maziwa Sinza lakini ukifika hayupo jambo ambalo linakupotezea muda na wala hajali lakini ndoto yangu ni siku moja kumiliki ng'ombe wangu ili niwe nakamua maziwa mwenyewe," anasema Omary.

